# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**ISO 9001:2015 Imethibitishwa**

## KODI NA USHURU MBALIMBALI 2025/2026



**JULAI, 2025**

***"KODI KWA MAENDELEO YETU"***

@Tanzania Revenue Authority

## MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

### DIRA

Taasisi ya Mapato inayoaminika kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi

### DHAMIRA

Tunarahisisha na kuimarisha ulipaji wa kodi wa hiari kwa maendeleo endelevu

### MANDHARI YA KIMKAKATI

Uboreshaji wa Utendaji,
Ushirikishwaji wa Walipakodi,
Matumizi ya Mifumo
na Ubunifu

### MAADILI YA MSINGI YA TRA

Weledi
Uadilifu
Uaminifu
Uwajibikaji

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 Imethibitishwa**

# KODI NA USHURU MBALIMBALI 2025/2026

## JULAI, 2025

# YALIYOMO

**A. KODI YA MOJA KWA MOJA ........................................................1**
1.0 Kodi ya Kampuni: ........................................................................1
2.0 Kodi ya Zuio:.................................................................................2
3.0 Pato litokanalo na Uuzaji wa rasilimali ...........................................4
5.0 Tozo ya mafunzo na maendeleo ya Ufundi Stadi (SDL).................7
6.0 Viwango vya Kodi ya mapato kwa wafanyabiashara binafsi wadogo wakazi ..........................................................................................8
8.0 Risiti za Kielektroniki..................................................................... 11
9.0 Uwasilishaji wa ritani na malipo ya Kodi ya Mapato.......................12
10.0 Madaraja ya Mali zinazopungua Thamani pamoja na Viwango vya punguzo la kikodi kwa kila mwaka: ...............................................17

**B. KODI YA MLAJI.........................................................................19**
11.0 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)............................................19
11.1 i) Watu Wanaopaswa Kusajiliwa kwa ajili ya VAT .........................19
11.2 Viwango vya VAT na Kodi ya Zuio la VAT....................................20
11.3 Mauzo yanayotozwa VAT kwa kiwango cha asilimia 0 (Zero-rated Supplies) ......................................................................20
11.4 Kiwango cha usajili wa VAT Zanzibar ...........................................24
11.5 Viwango vya VAT Zanzibar` .........................................................24
11.6 Uwasilishaji wa Ritani ya VAT na Malipo: ....................................24

**C. USHURU WA FORODHA ..........................................................25**
12. Ushuru wa Forodha wa Kuagiza Bidhaa kutoka Nje ya nchi..........25
13. Viwango vya Ushuru wa Bidhaa...................................................26
14. Utaratibu wa kodi ya usafirishaji bidhaa nje ya nchi.......................31
15. Kizuizi cha usafirishaji au matumizi ya ndani ya madini................31
16. Bidhaa zilizopigwa marufuku.........................................................31
17. Bidhaa zilizozuiliwa.......................................................................32

18. Ada ya Uchakataji wa Forodha:....................................................32
19.Uagizaji bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na SADC:........................................................32
20. Sheria ya Ushuru wa Pamoja wa Nje wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2022 na Sheria ya Usimamizi wa Forodha, 2004. .......33
21. Mabadiliko ya Viwango vya Ushuru wa Kuagiza/Kukaa kwa Maombi. 33
22.Ushuru wa Maendeleo ya Viwanda unaotozwa kwa thamani ya forodha ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ................................35
23. Ondoleo la wajibu. ..........................................................................37

**D. KODI NA TOZO NYINGINEZO ........................................................39**
24.. Ushuru wa Stempu ..........................................................................39
25. Kodi ya usajili na uhamisho wa magari ..........................................40
26. Viwango Vipya vya Usajili wa Kwanza wa Magari ya Umeme ......40
27 Ada za Uhamisho wa Magari..........................................................41
28. Leseni ya Uendeshaji wa Magari....................................................41
29 Utaratibu wa tozo ya barabara na mafuta .....................................41
30. Kodi za michezo ya kubahatisha ...................................................42
31. Marejesho ya Kodi .........................................................................43
32. Tozo, Ada, au Malipo toka Sekta ya Utalii .....................................43
33 Ada za Huduma za Bandari...........................................................44
34 Ushuru wa huduma ya Viwanja vya Ndege .................................44
35 Usimamizi wa Kodi .........................................................................44

## A. KODI YA MOJA KWA MOJA VIWANGO

| Na. | MAELEZO | MKAZI | WASIO MKAZI |
|---|---|---|---|
| **1.0 Kodi ya Kampuni:** | | | |
| (a) | Kiwango cha kodi kwa jumla ya Mapato ya kampuni | 30% | 30% |
| (b) | Kampuni isipogawanya faida yoyote ndani ya miezi 12 baada ya mwisho wa mwaka wake wa fedha, Kamishna wa TRA anaweza kuchukulia kwamba asilimia 30 ya faida ya Kampuni husika imegawanywa kwa wanahisa (hata kama hakuna mgawanyo halisi ulio fanyika), | 10% | N/A |
| c | Kampuni inayopata hasara kwa miaka 3 mfululizo bila kujumuisha kampuni linalofanya biashara ya kilimo, usindikaji wa chai, utoaji wa huduma za afya na elimu.<br>Kumbuka: Kwa kampuni linalofanya usindikaji wa chai, kifungu kilicho hapo juu kimeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2024 hadi tarehe 30 Juni, 2027 | 1% | N/A |
| d | Uuzaji wa mazao ya misitu ili kulipa kodi ya mapato kwa awamu moja kwa mtu binafsi, (Mbao, Magogo, Mirunda na Nguzo) kuanzia tarehe 1 Januari 2026 | 2% | N/A |
| (e) | Kampuni mpya iliyoorodheshwa katika Soko la Hisa na mitaji la Dar es Salaam (DSE), na angalau asilimia 25 ya umiliki wake umetolewa kwa umma kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia tarehe ya kuorodheshwa. | 25% | 25% |
| (f) | Kuongeza asilimia ya mapato yanayopaswa kutozwa kodi ambayo hayatapunguzwa na hasara zisizotarajiwa kutoka asilimia 30 hadi 40 katika sekta ya uziduaji. | 30% | N/A |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (g) | Kampuni mpya iliyonzishwa kwa ajili kutengeneza dawa au bidhaa za ngozi na kuwa na makubaliano ya utendaji na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania italipa kodi kwa kiwango kilichopunguzwa cha kampuni kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka wa kuanza kwa uzalishaji. | 20% | N/A |
| (h) | Jumla ya mapato ya Uanzishwaji wa Kudumu wa Ndani. | N/A | 30% |
| (i) | Kodi ya Huduma za kimtandao (DST) Malipo yanayopokelewa na mtu asiye mkaazi ambaye anatoa huduma za kielektroniki zinazotumiwa katika URT. | N/A | 2% |
| (j) | Mapato yaliyorejeshwa ya uanzishwaji wa kudumu wa ndani wa mtu ambaye sio mkazi | N/A | 10% |
| **2.0 Kodi ya Zuio:** | | | |
| (a) | (i) Malipo ya gawio yanayofanywa na kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es salaam | 5% | 5% |
| (b) | Malipo ya kamisheni kwa huduma ya uhamisho wa fedha, ada au tozo kuptia kwa: Mawakala wa Uhawilishaji Fedha, Mawakala wa Benki za Biashara, Mawakala wa Malipo ya Kidijitali, au kamisheni kwa huduma ya matangazo ya michezo ya kubahatisha. | 10% | N/A |
| (c) | Malipo ya Ununuzi wa madini ya Viwandani ikijumuisha Chumvi kutoka kwa PML au Wachimbaji Wadogo wasio rasmi. | 2% | N/A |
| (d) | Malipo ya gawio yaliyotolewa na kampuni nyingine | 10% | 10% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (e) | i) Malipo ya riba | 10% | 10% |
| | ii) Malipo ya riba kwa mmiliki wa hati fungani za kampuni au manispaa iliyotolewa na kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam kuanzia tarehe 1 Julai, 2022. | NIL | N/A |
| (f) | i) Malipo ya mrabaha | 15% | 15% |
| | ii) Malipo ya mrabaha yanatumika kwa tasnia ya filamu. | 10% | 10% |
| | iii) Malipo ya mrabaha kwa taasisi ya michezo au Shirikisho la Soka Tanzania | 5% | N/A |
| (g) | Malipo ya ada za Usimamizi na huduma za kiufundi (madini, mafutana gesi) | 5% | 15% |
| (h) | Malipo ya huduma za usafiri kwa wasio wakaazi mwendeshaji au mkodishaji bila uanzishwaji wa kudumu. Hii imesamehewa kwa Malipo yanayopokelewa kwa kubeba samaki au mazao ya kilimo cha maua na ndege ya kigeni. | N/A | 5% |
| (i) | i) Malipo ya kukodisha ardhi na majengo | 10% | 20% |
| | ii)Kukodisha Magari, Ndege binafsi, katika wigo wa zuio la kodi. | 10% | 15% |
| | iii) Malipo ya kukodisha kwa mitambo au mashine za ujenzi. | 10% | 10% |
| | iv) Mkazi au mtu asiye mkazi ambaye hufanya malipo kwa mtayarishaji wa maudhui ya kidijitali mkazi. | 5% | NA |
| | v) Mkazi au mtu asiye mkazi ambaye anamiliki jukwaa la kubadilishana mali ya kidijitali au kuwezesha ubadilishanaji au uhamishaji wa mali ya kidijitali na kufanya malipo kwa mkazi. | 3% | NA |
| | iv) Ukodisha mali nyingine | N/A | 15% |
| (k) | Malipo ya Bima | N/A | 10% |
| (l) | Malipo ya Maliasili | 15% | 15% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (m) | Malipo ya Kitaalamu na Huduma zingine | 10% | 15% |
| (n) | Malipo ya Ada kwa Wakurugenzi (Wakurugenzi wasiofanya kazi kwenye kampuni muda wote) | 15% | 15% |
| (o) | Malipo ya bidhaa zinazouzwa kwa Serikali au taasisi yoyote iliyofadhiliwa kwa kiasi kikubwa na Serikali | 2% | N/A |
| (p) | Malipo ya Ununuzi wa madini ya metali ya Thamani, madini ya Vito na Vito vinginevyo vya thamani kutoka kwa Wamiliki wa Leseni za Uchimbaji Mdogo wa madini (PML) au Wachimbaji Wadogo wasio rasmi. | 2% | N/A |
| (q) | Malipo yanafanywa kwa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa, misitu ya kijamii au mkazi yeyote kuhusiana na upunguzaji wa hewa ukaa uliothibitishwa | N/A | 10% |
| **Kumbuka:** **Kodi ya mapato ya zuio inayozuiliwa kwa watu tofauti na waliotajwa hapo juu itakuwa kodi ya mapato ya zuio isiyo ya mwisho** Uwasilishaji wa taarifa ya kodi iliyozuiwa na Malipo ya kodi ya zuio yanapaswa kuwa ndani ya siku 7 baada ya mwezi wa makato | | | |
| **3.0 Pato litokanalo na Uuzaji wa rasilimali** | | | |
| | **a) Ardhi na Majengo** | | |
| | i) Ardhi au Majengo kwa mtu ambaye ana kumbukumbu za gharama ya mali, ukokotoaji wa kodi utafanywa kwa kutegemea ziada iliyopatikana katika mauzo husika. | 10% | 30% |
| | ii) Ardhi au Majengo ambayo muuzaji ambaye ni mtu binafsi hana kumbukumbu za gharama alizotumia. Ukokotoaji wa kodi utafanywa kwa kutegemea kiasi kikubwa kati ya bei ya mauziano authamani iliyothibitishwa. | 3% | N/A |
| | iii) Haki miliki za mafuta au madini | 30% | 30% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | iv) Hisa au dhamana zinazomilikiwa na kampuni mkazi | 10% | 20% |
| | **b) Msamaha katika mauzo ya rasilimali** | | |
| | a) Makazi ya kibinafsi ambayo yamemilikiwa na kuishi kwa miaka mitatu au zaidi - Faida ya TZS 15 milioni au chini (Uuzaji wa nyumba ya makazi chini ya kiwango kilichowekwa)<br>b) Ardhi ya kilimo iliyotumika kwa angalau vipindi viwili vya kilimo ndani ya miaka 3 kabla ya uuzwaji wa ardhi hiyo na thamani ya soko ya ardhi ni chini ya TZS 10 milioni<br>c) **Hisa**- Hisa za DSE zinazomilikiwa na mtu mkazi au asiye mkazi kwa kwa kiwango kisichozidi 25%<br>d) Kiasi kinachotokana na faida kutokana na utekelezaji au uhamishaji wa haki za madini na taarifa za madini kwenda kwa taasisi ya ubia iliyoanzishwa kati ya Serikali na mwekezaji, au uhamishaji wa hisa zinazobebwa bila malipo, au uhamishaji wa hisa kwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina.<br>e) Uhamisho wa mali kati ya mume na mke<br>f) Uhamisho wa mali kwa sababu ya talaka au kutengana kisheria<br>g) Uhamisho wa mali kwa mwenzi au mwenzi wa zamani baada ya kifo<br>h) Uhamisho wa mali kwa wosia au urithi<br>i) Uuzaji/Uhamisho wa Hati-Fungani Fupi na Dhamana za Serikali<br>j) Uhamisho wa ndani ya kampuni au uhamisho uliosababishwa na mabadiliko ya muundo mpya wa kampuni kama ulivyo idhinishwa na Kamishna Mkuu wa TRA | | |

## 4.0 Kodi ya Mapato ya Mtu Binafsi (Tanzania Bara na Zanzibar)

| Mapato ya Kila Mwezi | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|
| Ambapo mapato yote hayazidi TZS 270,000/= | HAKUNA KODI |
| Ambapo mapato yote yanazidi TZS 270,000 lakini hayazidi TZS 520,000/= | 8% ya kiasi kinachozidi TZS 270,000/= |

| | |
|---|---|
| Ambapo mapato yote yanazidi TZS 520,000 lakini hayazidi TZS 760,000/= | TZS 20,000/= pamoja na 20% ya kiasi kinachozidi TZS 520,000/= |
| Ambapo jumla ya mapato yanazidi TZS 760,000/=lakini haizidi TZS 1,000,000/= | TZS 68,000/= pamoja na 25% ya kiasi kinachozidi TZS 760,000/= |
| Ambapo jumla ya mapato yanazidi TZS 1,000,000/= | TZS 128,000/= pamoja na 30% ya kiasi kinachozidi TZS 1,000,000/= |

**Vidokezo:**

- ✓ Mapato ya Mwaka ya TZS 3,240,000/= hayatozwi kodi
- ✓ Mfanyakazi anayetoa misaada kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu, mchango huo ni gharama zinazoruhusiwa kutokana na kodi. Hata hivyo, mchango huo ni baada ya kuidhinishwa na Kamishna
- ✓ Malipo yanayolipwa kwa mfanyakazi asiye mkazi wa mwajiri mkazi yatatozwa kosi ya zuio wa 15%.
- ✓ Jumla ya mapato ya mtu ambaye si mkazi hutozwa kwa kiwango cha 30%
- ✓ Mfanyakazi aliye na ajira ya ziada anatozwa kwa kiwango cha 30%.
- ✓ Uwasilishaji wa ritani na Malipo ya kiasi kilichozuiliwa kutokana na ajira ni ndani ya siku 7 baada ya mwezi unaofuata.
- ✓ Mfanyakazi ambaye si mkazi ambaye mapato yake kwa mwaka wa mapato yanajumuisha mapato kutoka kwa ajira pekee hayaruhusiwi kuwasilisha ritani.

| **4.1** | **Manufaa yatokanayo na Ajira** |
|---|---|
| **(a)** | **Utoaji wa Majengo pamoja na samani**<br>Ukokotoaji wa marupurupu ya mwajiriwa kutokana na nyumba aliyopewa na mwajiri yatazingatia bei ambayo ni ndogo kati ya bei ya soko na ile inayozidi yafuatayo:-<br>i) Kubwa zaidi ya<br>(a) 15% ya mapato yote ya ajira ya mwaka ya mwajiriwa na<br>(b) Matumizi yanayodaiwa na mwajiri juu ya jengo. |

| (b) | **Matumizi ya Gari**<br>Manufaa yake yanategemea uwezo ya injini ya Gari na umri wa gari tangu lilipotengenezwa kama ifuatavyo. |
|---|---|

| **Ukubwa wa Injini ya Gari** | **Chini ya miaka 5** | **Umri zaidi ya miaka 5** |
|---|---|---|
| Haizid icc 1000 | TZS 250,000/= | TZS 125,000/= |
| Zaidi ya 1000 cc lakini haizidi 2000 cc | TZS 500,000/= | TZS 250,000/= |
| Zaidi ya 2000 cclakini haizidi 3000 cc | TZS 1,000,000/= | TZS 500,000/= |
| Juu 3000 cc | TZS 1,500,000/= | TZS 750,000/= |

## 5.0 Tozo ya mafunzo na maendeleo ya Ufundi Stadi (SDL)

(i) Tanzania Bara kiwango ni 3.5% ya malipo yote aliyolipa mwajiri kwa wafanyakazi wake kwa mwezi husika. Mwajiri anapaswa kuwa na wafanyakazi kuanzia 10 ili kulipa kodi hii.

ii) Kiwango ni 4% ya mapato ya kila mwezi kwa Tanzania Zanzibar. Inalipwa na mwajiri aliye na wafanyikazi 4 au zaidi

ii) Ritani itawasilishwa na mwajiri mwenye sifa ya kulipa SDL.

**Waajiri Wameondolewa kwenye Malipo ya SDL**

a) Idara au Taasisi ya Umma ambayo inafadhiliwa kikamilifu na Serikali

b) Mwanadiplomasia na Misheni

c) Umoja wa Mataifa na Taasisi zake

d) Taasisi za kimataifa na nyingine za kigeni zinazohusika na misaada au usaidizi wa kiufundi

e) Mamlaka ya Serikali za Mitaa

f) Taasisi za kidini ambazo Wafanyikazi wake wameajiriwa pekee kusimamia maeneo ya ibada, kutoa maagizo ya kidini au kwa ujumla kuhudumu dini na utoaji wa afya ya umma.

g) Mashirika ya hisani

h) **Wanafunzi wa ndani kutoka vyuo vya elimu ya juu** au kiufundi na elimu ya ufundi na taasisi za mafunzo ambao wako chini ya mpango wa Wakala wa Huduma ya Ajira Tanzania

i) Waajiri wa mashambani ambao wafanyakazi wao wanajishughulisha na kilimo moja kwa moja na pekee

j) Shule za Taasisi za elimu zilizosajiliwa zikiwemo Nursery, Msingi na Sekondari; Shule za Ufundi, Elimu na Mafunzo; wanafunzi waliohitimu kutoka vyuo vya elimu ya juu.

k) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira kuhusu Malipo ya Wafanyakazi wa Kawaida wanaojishughulisha na utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira.

l) Waziri mwenye dhamana ya fedha anaweza, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya elimu na kwa amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kumuachia mtu yeyote kulipa SDL.

**Kumbuka:**

- ✓ Mapato ya jumla ni pamoja na mshahara, malipo ya likizo, likizo ya ugonjwa, malipo badala ya likizo, kamisheni ya ada, takrima, bonasi, posho zozote za kujikimu, za kusafiri au burudani.
- ✓ Misamaha kwa Zanzibar inatumika tu kuanzia (a) hadi e) hapo juu.
- ✓ Uwasilishaji wa ritani na Malipo ya SDL inapaswa kufanywa ndani ya siku saba (7) baada ya mwezi wa malipo.

### 6.0 Viwango vya Kodi ya mapato kwa wafanyabiashara binafsi wadogo wakazi

| ***Mauzo ya kila mwaka*** | ***Kodi kwa asiye-tunza Kumbukumbu*** | ***Kodi kwa anayetunza Kumbukumbu*** |
|---|---|---|
| Ambapo mauzo hayazidi TZS 4,000,000/= | NIL | NIL |
| Ambapo mauzo yanazidi TZS 4,000,000/= na lakini hayazidi 7,000,000/= | TZS 100,000/= | 3% yamauzo ya zaidi ya TZS 4,000,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| Ambapo mauzo yanazidi TZS 7,000,000/= lakini hayazidi TZS 11,000,0000/= | TZS 250,000/= | TZS 90,000/= pamoja na 3% ya mauzo zaidi ya TZS 7,000,000/= |
| Ambapo mauzo ni kati ya TZS 11,000,001/=na TZS 100,000,000/= | | 3.5% ya mauzo |

**7.0 Viwango vya kodi ya mapato kwa mkazi anayehusika na usafirishaji wa abiria au bidhaa**

**Daraja A : Magari ya Kuhudumia Abiria**

| Idadi ya Abiria | Malipo ya Kodi |
|---|---|
| 1 hadi 5 | 120,000 |
| 6 hadi 15 | 250,000 |
| 16 hadi 30 | 650,000 |
| 31 hadi 45 | 1,100,000 |
| 46 hadi 65 | 1,600,000 |
| Juu ya 65 | 2,200,000 |

**Daraja B: Magari ya Huduma ya Utalii**

| Idadi ya Watalii | Kodi Inalipwa |
|---|---|
| 1 hadi 15 | 650,000 |
| 16 hadi 25 | 900,000 |
| 26 hadi 45 | 1,300,000 |
| 46 hadi 65 | 1,800,000 |
| Juu ya 65 | 2,400,000 |

| Daraja C: Magari ya Mizigo | |
|---|---|
| **Uwezo (Tani)** | **Kodi Inalipwa** |
| Hadi kilo 500 | 120,000 |
| Zaidi ya kilo 500 hadi tani 1 | 250,000 |
| 1 hadi tani 5 | 500,000 |
| 6 hadi 10 tani | 750,000 |
| tani 11 hadi 15 | 1,100,000 |
| tani 16 hadi 20 | 1,300,000 |
| tani 21 hadi 25 | 1,650,000 |
| tani 26 hadi 30 | 1,900,000 |
| Zaidi ya 30 | 2,200,000 |
| **Daraja D: Magari ya Huduma ya Kukodisha Binafsi** | |
| **Jamii ya Magari** | **Kodi Inalipwa** |
| Teksi | 180,000 |
| Panda Hailing | 350,000 |
| Kushiriki kwa Safari | 450,000 |
| Ajira Maalum | 750,000 |

**Kumbuka:**

- Mtu binafsi ambaye ana mauzo zaidi ya TZS 100,000,000/= kwa mwaka, analazimika kuandaa Hesabu za Mizania zilizokaguliwa za biashara yake na kuwasilisha ritani ya Mapato.
- Mtu ambaye mauzo yake ni TZS 11,000,000/= au zaidi atatoa risiti ya kieletroniki.
- Mtu ambaye mauzo yake ni chini ya TZS 11,000,000/= atatoa stakabadhi ya maandishi kwa nakala iliyo na maelezo ya:- tarehe, jina kamili la mtu aliyeuziwa bidhaa pamoja na TIN, maelezo kamili ya bidhaa, jina kamili na anwani ambaye bidhaa hizo ziliuzwa.
- Viwango vya wafanyabiashara wadogo havihusishi wataalamu,

taaluma, wakurugenzi, tasnia ya ujenzi na tasnia ya mafunzo.

- Marejesho ya mapato ya mtu ambaye mauzo yake katika mwaka wa mapato yanazidi milioni 500 au kampuni ambayo mapato yake ya jumla yanazidi 100m yanapaswa kutayarishwa au kuthibitishwa na CPA -PP.

## 8.0 Risiti za Kielektroniki

- ❖ Mtu anayeuza bidhaa au kutoa huduma ambaye mauzo yake yanazidi TZS 11,000,000/= kwa mwaka atalazimika kutoa risiti za kielektroniki
- ❖ Mtu ambaye atashindwa kutoa risiti ya kielektroniki au kutoa risiti ya kielektroniki ambayo ni ya uongo au isiyo sahihi anatenda kosa na atawajibika; faini yoyote kubwa kati ya TZS 2,000,000.00 au 20% ya thamani ya bidhaa zinazouzwa au huduma zinazotolewa, na kwamba, faini haitazidi TZS 4,000,000.00, au atawajibika kwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu au voyote kwa pamoja.
- ❖ Mtu yeyote ambaye atashindwa kudai risiti za kielektroniki baada ya kupokea bidhaa au huduma au malipo ya bidhaa au huduma atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini ya asilimia 20 ya kodi iliyokwepa au TZS 40,000.00, kutegemea ni ipi kubwa zaidi.
- ❖ Matumizi yaliyofanywa na mtu katika mwaka wa mapato kwa bidhaa au huduma zinazohusiana na uzalishaji wa mapato yatasaidiwa na risiti ya kielektroniki isipokuwa pale ambapo mtu anayetoa bidhaa au huduma-

  (a) ni mtu asiye mkazi asiye na uanzishwaji wa kudumu katika Jamhuri ya Muungano; au

  (b) haijajumuishwa katika sharti la kutoa risiti ya kielektroniki

## 9.0 Uwasilishaji wa ritani na malipo ya Kodi ya Mapato

### (a) Ritani za Kodi ya Mapato

| Tarehe za Kukamilika kwa Uwasilishaji wa ritani ya Kodi ya Mapato | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina ya Wajibu** | **Nani Anawasilisha / Analipa** | **Tarehe ya Mwisho** | **Ufafanuzi Wazi kwa Walipakodi** |
| **Taarifa ya Makadirio ya Kodi ya Kulipwa (SOETP)** | Walipakodi wote wenye mapato yanayopaswa kutozwa Kodi ya Mapato (Kampuni, Wataalamu, Biashara) | **Ndani ya miezi 3** kuanzia mwanzo wa mwaka wa mapato | Tangaza mapato na kodi unayotarajia kwa mwaka ndani ya miezi 3 baada ya kuanza mwaka. |
| **Malipo ya Kodi kwa kila Awamu ya Robo Mwaka** | Walipakodi waliowasilisha SOETP | **Kabla au mnamo siku ya mwisho ya mwezi wa 3, 6, 9 na 12** ya mwaka wa mapato | Lipa makadirio ya kodi katika awamu nne katika mwaka. |
| **Ritani ya Mapato ya Mwaka (ROI)** | Kampuni, Biashara za Ubia, na miundo mingineyo ya biashara | **Ndani ya miezi 6** baada ya mwisho wa mwaka wa Fedha | Rejesha mapato ya mwisho ndani ya miezi 6 baada ya mwisho wa mwaka. |
| **Salio la Mwisho la Kodi ya Mapato** | Kampuni, Biashara za Ubia, na miundo mingineyo ya biashara | Pamoja na ROI, yaani ndani ya miezi 6 baada ya mwisho wa mwaka wa Fedha | Lipa salio lolote la kodi ya Mapato ambalo halikulipwa katika utaratibu wa malipo kodi ya mapato kwa awamu. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Ritani ya Mapato ya Mwaka (ROI) – Kwa Taasisi za Serikali** | Wizara, Idara, Wakala, Halmashauri za Wilaya na Miji, Taasisi nyinginezo za Umma | **Septemba 30** baada ya mwisho wa mwaka wa Fedha | Taasisi za serikali lazima yawasilishe marejesho yao ya kila mwaka kabla ya tarehe 30 Sept. |
| **Salio la Mwisho la Kodi ya Mapato kwa Taasisi za Serikali** | Wizara, Idara, Wakala, Halmashauri za Wilaya na Miji, Taasisi nyinginezo za Umma | **Kabla au Mnamo Septemba 30 baada ya Mwisho wa Mwaka wa Fedha** | Kiasi chochote cha Kodi ya Mapato kinacho daiwa lazima ilipwe wakati wa kuwasilisha ritani ya Mwisho wa Mwaka. |

Mtu ambaye atashindwa kuwasilisha ritani ya kodi kwa tarehe inayotarajiwa atawajibika kwa adhabu ya kila mwezi au sehemu ya mwezi ambapo kushindwa kuwasilisha.
Adhabu ni;

**Katika kesi ya mtu binafsi:** 2.5% ya kiasi cha kodi kinachokadiriwa au TZS100,000 chochote kilicho juu zaidi

**Katika kesi ya chombo:** 2.5% ya kiasi cha kodi kinachokadiriwa au TZS300,000 chochote kilicho juu zaidi.
Ucheleweshaji wa malipo ya kodi: Itatozwa riba kwa kiwango cha kisheria cha Benki Kuu ya Tanzania (BOT) wakati wa kutoza.

### b) Tarehe za mwisho za kuwasilisha ritani na kulipa kodi

| Na. | Aina ya Kodi/Ushuru | Ukomo wa Tarehe za kuwasilisha Ritani | Ukomo wa Tarehe za Kuanya Malipo ya Kodi | Ufafanuzi kwa Walipa Kodi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Kodi ya Mapato ya Kampuni (CIT)** | Ritani ya mwisho (ROI): Ndani ya **miezi 6** baada ya kumalizika kwa mwaka wa Biashara | Malipo ya awamu **kila baada ya miezi 3** (Kabla au mwisho wa mwezi wa 3, mwezi wa 6, mwezi wa 9 & mwezi wa 12); baki ndani ya kipindi cha miezi 6 baada ya mwisho wa mwaka | Kampuni hulipa kwa awamu za robo mwaka. Mwisho wa mwaka, hufanya hesabu ya mwisho na kulipa salio ndani ya miezi 6. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | **Kodi ya Mapato ya Binafsi** | Mtu binafsi anatakiwa kuwasilisha **Ritani ya Mapato (SOETP)** iwapo ana **mapato zaidi ya mshahara** (mfano biashara, nyumba za kupangisha, uwekezaji n.k.) au kama **mapato yake hayajakamilika** kwa mfumo wa **PAYE** au **kodi ya mwisho (final withholding tax)** Lakini **si lazima** kwa Mtu Binafsi kuwasilisha ROI endapo mtu binafsi ana **ajira pekee** na kodi yake yote inakatwa moja kwa moja kupitia **PAYE** na kukabidhiwa TRA na mwajiri wake. | Malipo ya awamu **kila baada ya miezi 3**; baki ndani ya kipindi cha miezi 6 baada ya mwisho wa mwaka yaani, kabla ya 30 Juni ya mwaka wa Kalenda unaofuata. | Walipakodi binafsi hulipa kwa awamu na kulipa baki baada ya mwaka wa mapato. |
| 3 | **Kodi ya Ongezeko la Mtaji (Capital Gain Tax (CGT))** | Papo hapo wakati wa uhamisho wa mali | Ndani ya **siku 30** tangu uhamisho | Kodi hii hutozwa wakati wa kuuza mali/shares. Hulipwa mara moja baada ya muamala. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | **Kodi ya Mapato ya Zuio (Withholding Tax - WHT)** | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Wanaozuilia (waajiri au walipaji) lazima wapeleke kodi TRA ifikapo tarehe 7 ya mwezi unaofuata. |
| 5 | **P.A.Y.E (Pay As You Earn)** | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Waajiri wanakata PAYE kwenye mishahara ya wafanyakazi na kuwasilisha TRA kila mwezi. |
| 6 | **Kodi ya Huduma za Kidijitali (DST)** | Kabla au ifikapo **tarehe 20** ya mwezi unaofuata | Kabla au ifikapo **tarehe 20** ya mwezi unaofuata | Majukwaa ya kidijitali (ya ndani au ya kigeni) lazima yawasilishe na kulipa kila mwezi. |
| 7 | **Ada ya Maendeleo ya Ujuzi (SDL)** | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Waajiri huchangia kila mwezi kusaidia mafunzo ya wafanyakazi. |
| 8 | **Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)** | Kabla au ifikapo **tarehe 20** ya mwezi unaofuata; **TAMBUA:** Kama ilivyorekebishwa na **Sheria ya fedha, 2025;** Mlipakodi **hatapewa tena muda wa nyongeza** moja kwa moja endapo tarehe ya kuwasilisha ritani **itaangukia siku ya mapumziko au siku isiyo ya kazi**. | Kabla au ifikapo **tarehe 20** ya mwezi unaofuata | Wafanyabiashara waliosajiliwa kwa VAT wanawasilisha na kulipa kila mwezi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9 | **Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty)** | Kabla au ifikapo **tarehe 25** ya mwezi unaofuata. | Kabla au ifikapo **tarehe 25** ya mwezi unaofuata | Hutozwa kwenye bidhaa na huduma kama pombe, tumbaku, mafuta, simu n.k. |
| 10 | **Ushuru wa Stempu (Stamp Duty)** | Hakuna mfumo wa kuwasilisha ritani za kila mwezi au kila mwaka. | Malipo hufanyika mara moja baada ya kusainiwa au kupokelewa kwa nyaraka, mradi usizidi **siku 30** za kutimiza sharti la kisheria. | Ushuru wa Stempu hulipwa mara tu kila muamala (mfano uhamisho wa mali, mikataba) unapofanyika |
| 11 | **Kodi za Michezo ya Kubahatisha (Gaming Taxes)** | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Kabla au ifikapo **tarehe 7** ya mwezi unaofuata | Hutozwa kwa kampuni za michezo ya kubahatisha, bahati nasibu na betting. |
| 12 | **Ada ya Huduma za Uwanja wa Ndege** | Ada hukusanywa wakati wa kuuza tiketi na Ritani huwasilishwa TRA kabla ya **tarehe 20** ya mwezi unaofuata | Kuwasilishwa TRA kabla ya **tarehe 20** ya mwezi unaofuata | Mashirika ya ndege/mawakala hukusanya kutoka kwa abiria na kuwasilisha TRA kila mwezi. |
| 13 | **Ada ya Huduma za Bandari** | Ada hukusanywa wakati wa kuuza tiketi na Ritani huwasilishwa TRA kabla au ifikapo **tarehe 20** ya mwezi unaofuata | Kabla au ifikapo **tarehe 20** ya mwezi unaofuata | Mawakala wa usafirishaji hukusanya kutoka kwa abiria na kuwasilisha TRA kila mwezi. |

**Maelezo ya Haraka**

- **Tarehe 7 ya mwezi unaofuata -** PAYE, WHT, DST, SDL, na Kodi za Michezo ya Kubahatisha.
- **Tarehe 20 ya mwezi unaofuata -** VAT, Ada za Uwanja wa Ndege na Ada za Bandari.

- **Tarehe 25 ya mwezi unaofuata -** Ushuru wa Bidhaa
- **Tarehe Maalum -** CIT & Kodi ya Mapato ya Binafsi (malipo ya awamu + ritani ya mwisho), CGT (ndani ya siku 30 baada ya mauzo), Stamp Duty (kila Muamala), Airport Charges (wakati wa Kukata Tiketi).

## 10.0 Madaraja ya Mali zinazopungua Thamani pamoja na Viwango vya punguzo la kikodi kwa kila mwaka:

| Daraja | Mali Zinazojumuishwa | Kiwango cha Punguzo | Mifano |
|---|---|---|---|
| **1** | Kompyuta na vifaa vya kushughulikia data (pamoja na vifaa); Magari, mabasi madogo na mabasi (<30 viti); Magari ya bidhaa (< tani 7); Vifaa vya ujenzi na Mitambo ya uchimbaji na uhamishaji udongo. | **37.5%** (hukokotolewa kwa mbinu ya salio linalopungua) | Kompyuta mpakato , Toyota Prado, basi la watu 25, Tingatinga |
| **2** | Mabasi (≥30 viti); Malori mazito; Malori maalum; Trela na vyombo vilivyopachikwa trela; Magari ya reli na injini za treni; Vyombo vya usafiri majini kama vile meli, majahazi, tug na vyombo vinginevyo mfano wa hivyo **--** usafiri sawa wa maji; Ndege; Magari mengine yanayojiendesha yenyewe; Kilimo/Mitambo ya uzalishaji utengenezaji; Viwanda/Mitambo Maalum ya huduma; Mitambo ya umwagiliaji. | **25%** (hukokotolewa kwa mbinu ya salio linalopungua) | Scania basi, meli ya mizigo, mitambo ya kiwandani, mfumo wa umwagiliaji |
| **3** | Samani za ofisi, vifaa vya kudumu vya ofis na kipengee chochote cha mali ambacho hakijajumuishwa katika daraja lingine. | **12.5%** ( hukokotolewa kwa mbinu ya salio linalopungua ) | Madawati, viti, rafu, vichapishaji |
| **4** | [Imefutwa] | - | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **5** | Majengo ya kudumu, miundombinu na kazi za ujenzi za kilimo, ufugaji wa mifugo au ufugaji wa samaki. | **5%**( hukokotolewa kwa mbinu ya mstari wima ) | Mazizi, mabanda ya ng'ombe, mabwawa ya samaki |
| **6** | Majengo, miundo na kazi za ujenzi za kudumu isipokuwa zile za daraja la 5. | **5%**( hukokotolewa kwa mbinu ya mstari wima) | Majengo ya ofisi, maghala, viwanda |
| **7** | Mali zisizoshikika (thamani ya sifa ya biashara, hataza, hakimiliki, alama za biashara, programu, n.k.). | **Imepunguzwa kwa 12.5%** ( hukokotolewa kwa mbinu ya mstari wima ) | Alama ya biashara, thamani ya sifa ya biashara, leseni ya programu |
| **8** | Mali maalum ya motisha: Mitambo na mashine kwa ajili ya kilimo; Vinu vya upepo, jenereta za umeme na vifaa vya usambazaji kwa ajili ya kilimo; Electronic Fiscal Devices (EFDs) zilizonunuliwa na wafanyabiashara wasiosajiliwa kwa ajili ya VAT; Vifaa vya utafutaji na uchunguzi awali wa madini/petroli. | **Kiwango kilichobainishwa na sheria (**kwa ujumla 100% ya pinguzo la kodi linaloruhusuwa kwa mara moja mwanzoni katika mwaka wa kwanza kwa matumizi ya mali husika, kabla na kuendelea na punguzo za kawaida za thamani ya mali hiyo (**normal capital aallowances**) punguzo la kikodi la awali au 50% kulingana na masharti ya Sheria ya Kodi ya mapato**)** | Windmill, pampu ya umwagiliaji, mashine ya EFD, mitambo ya uchunguzi wa madini |

# B. KODI YA MLAJI

## 11.0 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

**11.1 i) Watu Wanaopaswa Kusajiliwa kwa ajili ya VAT**

- o Wale ambao kwa kufaa wanatarajia kufikia kiwango cha usajili wa VAT katika mwaka huu
- o Wale ambao tayari wamepata kizingiti katika miezi 12 iliyopita
- o Wale ambao walipata nusu ya kizingiti katika miezi 6 iliyopita

ii) **Watoa Huduma za Kitaalam**

- o Mfanyabiashara yeyote anayetoa huduma za kitaalamu Tanzania Bara

iii) **Taasisi za Serikali**

- o Chombo chochote cha serikali au taasisi inayofanya shughuli za kiuchumi

iv) **Wafanyabiashara wa VAT tarajiwa (Wawekezaji bado hawajaanza uzalishaji)**

- o Wawekezaji ambao wanataka kujiandikisha kabla ya kuanza uzalishaji ili waweze kudai VAT kwa gharama za kuanza.
- o Hawa wanalazimika Kuthibisha yafuatayo; -
  - ☐ Ushahidi wa Dhamiara ya kusajiliwa (kwa mfano, mikataba, zabuni, mipango ya ujenzi/biashara, vifaa vya ufadhili).
  - ☐ Uthibitisho Kwamba watazalisha bidhaa au huduma zitakazotozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani
  - ☐ Muda ulio wazi wa juu ya lini uzalishaji au huduma zinazotozwa VAT utaanza.

v) **Usajili wa Lazima**

Kamishna Mkuu wa TRA anaweza kumsajili Mfanyabiashara kwa lazima iwapo atashindwa kujisajiri kwa hiari au kwa maslahi ya kulinda mapato ya nchi

vi) **Usajili wa VAT uliorahisishwa** (Kwa watoa Huduma za Kielektroniki Wasio-Wakaazi)

- ☐ Kwa watoa Huduma za Kielektroniki Wasio-Wakaazi (kwa mfano, utangazaji, utiririshaji mtandaoni, mitandao ya kijamii).
- ☐ Hutumika pale ambapo kuteua Mwakilishi wa VAT nchini

Tanzania ni vigumu.

- **Hakuna Kiwango cha kizingiti cha usajili wa VAT kinachohitajika** katika kundi hili

| **11.2 Viwango vya VAT na Kodi ya Zuio la VAT** | |
|---|---|
| **Maelezo ya bidhaa/vifaa nahuduma** | **Viwango vya VAT** |
| Mauzo ya bidhaa na huduma yaliyofanyika Tanzania Bara | 18% |
| Bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi | 18% |
| Malipo ya ununuaji wa bidhaa au huduma kwa mlaji wa mwisho ambaye hajasajiliwa na VAT anapofanya malipo kupitia benki au mfumo wa malipo wa kielektroniki ulioidhinishwa na Kamishna Mkuu.(Kiwango cha punguzo). | 16% |
| Viwango vya kuzuia VAT kwenye chanzo cha malipo (VAT Withholding) | |
| Wakala aliyeidhinishwa kuzuia VAT atazuia VAT kutoka kwa wauzaji wa bidhaa na kuituma moja kwa moja kwa TRA. | 3% |
| Wakala aliyeidhinishwa kuzuia VAT atazuia VAT kutoka kwa wauzaji wa huduma na kuituma moja kwa moja kwa TRA. | 6% |

### 11.3 Mauzo yanayotozwa VAT kwa kiwango cha asilimia 0 (Zero-rated Supplies)

| **Bishaa/ Huduma inayohusika** | **Vigezo na Masharti ya kutozwa VAT kwa kiwango cha asilimia 0** | **Muda wa Kutumika kiwango 0%** |
|---|---|---|
| Mali isiyohamishika | Ardhi iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano | Inaendelea |
| Bidhaa | Bidhaa zinazosafirishwa nje (kama inavyofafanuliwa chini ya kifungu cha 2 cha Sheria ya VAT) | Inaendelea |

| | | |
|---|---|---|
| Bidhaa | Mauzo yaliyofanywa na muuzaji aliyeidhinishwa kuuza bidhaa bila kutza VAT kwa ajili ya mtalii au mgeni aliyedhibitwa kwamba bidhaa ailzo uziwa zitaondolewa katika Jamhuri ya Muunganio bila kutumika ndani ya nchi. | Inaendelea |
| Dhahabu | Mauzo dhahabu yayaliyofanywa kwa Benki Kuu ya Tanzania | Inaendelea |
| Dhahabu | Mauzo ya dhahabu yayaliyofanywa kwa wasafishaji wa dhahabu walio idhinishwa kwa kazi hiyo Tanzania Bara | Inaendelea |
| Mbolea | Mauzo ya mbolea iliyotengenezwa hapa nchini | 1 Julai 2025 - 30 Juni 2028 |
| Mavazi | Mauzo ya nguo zinazotengenezwa nchini kwa kutumia pamba inayozalishwa hapa nchini | 1 Julai 2025 - 30 Juni 2026 |
| Bidhaa (iliyokodishwa au iliyoidhinishwa kwa kibali maalum, nk) | Malipo ya kukodisha mali au bidhaa zinazoenda kutumika nje ya Jamhuri ya Muungano | Inaendelea |
| Bidhaa zilizokodishwa katika eneo la Kimataifa | Malipo ya Mali au bidhaa zilizokodishwa katika eneo la Kimataifa | Inaendelea |
| Njia za usafiri | Malipo ya Mali au bidhaa zilizokodishwa kwa ajili ya kutumika nje ya nchi kwa kipindi cha Zaidi ya siku thelethini | Inaendelea |

| | | |
|---|---|---|
| Bidhaa zilizo uzwa kwa ajili ya ukarabati wa bidhaa zilizo ingizwa nchini kwa muda | Bidhaa zilizo uzwa kwa ajili ya ukarabati wa bidhaa zilizo ingizwa nchini kwa muda (temporary imports) kwa maharti yafuatayo: (a) bidhaa zitakuwa sehemu ya/ zimeambatanishwa na uagizaji wa muda mfupi, au zinatumiwa wakati wa ukarabati; (b) uagizaji wa muda mfupi uko chini ya utaratibu wa EAC-CMA, huondolewa baada ya huduma, hazitumiki ndani isipokuwa kutekeleza huduma. | Inaendelea |
